JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

NA. 7 YA 2012

NAKUBALI,

JAKAYA MRISHO KIKWETE,
*Rais*

10 Oktoba, 2013

# Sheria itakayofanya Marekebisho katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83.

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tafsiri
Sura ya 83

**1.** Muswada huu utaitwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, mwaka 2013 utasomwa pamoja na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, ambayo itajulikana katika Sheria hii kama "Sheria mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3

**2.** Sheria mama inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 3 kwa kuingiza katika mtiririko wa kialfabetiki tafsiri mpya zifuatazo:–

"Rasimu ya Katiba" maana yake ni Rasimu ya Katiba ambayo imetayarishwa na Tume chini ya Sheria hii;

"Kanuni" maana yake ni Kanuni za Bunge Maalum zilizotungwa chini ya Sheria hii".

Marekebisho ya kifungu cha 20

**3.** Sheria mama inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 20 kwa kufuta kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake kifungu kifuatacho:

> "(4) Bila kujali kuvunjwa kwa Tume chini ya kifungu cha 37(1), Katibu wa Bunge Maalum anaweza, kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Bunge Maalum, kumwalika Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe yeyote wa Tume ilivyovunjwa ili kutoa ufafanuzi unaoweza kuhitajika wakati wa mjadala wa Bunge Maalum."

Marekebisho ya kifungu cha 22

**4.** Sheria mama inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 22 kwa:

(a) kufuta maneno ya utangulizi kwenye aya (c) yanayojitokeza katika kifungu kidogo cha (1) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

"(c) wajumbe mia moja sitini na sita watakaoteuliwa na Rais kwa kukubaliana na Rais wa Zanzibar kutokana na wafuatao;"

(b) kufuta aya (vi) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

"(vi) Shirikisho la Wafanyakazi";

(c) kuongeza baada ya kifungu kidogo cha (2), vifungu vifuatavyo:

"(2A) Rais ataalika kila kundi lililoainishwa katika kifungu kidogo cha (1)(c) kuwasilisha kwake orodha ya majina ya watu wasiozidi tisa kwa madhumuni ya uteuzi wa watu watatu kutoka kwenye orodha kuwa Wajumbe wa Bunge Maalum:

Isipokuwa kwamba, orodha hiyo itaonyesha, kwa kila jina linalopendekezwa, umri, jinsi, uzoefu, sifa na mahali anapotoka mtu huyo.

(2B) Katika kuteua wajumbe wa Bunge Maalum chini ya kifungu kidogo cha (1)(c), Rais atazingatia:

(a) sifa na uzoefu wa watu waliopendekezwa; na

(b) usawa wa kijinsia."

Kuongeza kifungu cha 22A

**5.** Sheria Mama inarekebishwa kwa–

(a) kuongeza baada ya Kifungu cha 22 Kifungu kipya kama ifuatavyo:

"Mwenyekiti wa muda

22A.-(1) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 23, baada ya kuitishwa kwa Bunge Maalum, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu wa Baraza la Wawakilishi watasimamia mchakato wa kumchagua Mwenyekiti wa muda wa Bunge Maalum atakayesimamia na kuongoza Bunge Maalum kwa madhumuni ya–

(a) kusimamia uandaaji na upitishwaji wa Kanuni za Bunge Maalum; na

(b) kuendesha uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum,

(2) Mwenyekiti wa muda aliyechaguliwa na Bunge Maalum chini ya kifungu kidogo cha (1) hatakuwa na sifa ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa Bunge Maalum."

**6.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 23 kwa- Marekebisho ya kifungu cha 23

(a) kuongeza baada ya kifungu kidogo cha (3) kifungu kifuatacho:

"(4) Mjumbe wa Bunge Maalum hatastahili kuteuliwa au kugombea nafasi ya kuwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti isipokuwa kama Mjumbe huyo-

(a) amehitimu shahada kutoka katika Chuo Kikuu kinachotambulika;

(b) amethibitika kuwa na uzoefu na ujuzi wa kuongoza mihadhara au mabaraza;

(5) Utaratibu wa maombi, uteuzi na uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu wa Mwenyekiti utakuwa kama utakavyoainishwa kwenye Kanuni."

(b) kubadilisha kifungu kidogo cha (4),(5) na (6) kuwa kifungu kidogo cha (6), (7) na (8) ipasavyo.

(c) hajawahi kutiwa hatiani na Mahakama yoyote katika Jamhuri ya Muungano na kuhukumiwa kifungo kisichozidi miezi sita kwa kosa lolote linalohusu kukosa uaminifu na maadili.

**7.** Sheria Mama inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 24 kwa– Marekebisho ya kifungu cha 24

(a) kufuta kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake kifungu kifuatacho:-

"(4) Katibu wa Bunge Maalum baada ya kushauriana na Naibu Katibu na taasisi za umma, atachagua idadi ya watumishi kutoka miongoni mwa watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Baraza la Wawakilishi, Ofisi za Wanasheria wa Jamhuri ya Muungano na Zanzibar na taasisi nyingine za umma kwa kadri itakavyohitajika kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge Maalum.

(5) Watumishi waliochaguliwa chini ya Kifungu kidogo cha (4), watakuwa katika masharti ya kuazimwa katika kipindi chote cha Bunge Maalum."

(b) kubadilisha kifungu kidogo cha (5) kuwa kifungu kidogo cha (6).

Marekebisho ya kifungu cha 26

**8.**-(1) Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 26 kwa kuongeza baada ya kifungu kidogo cha (2) vifungu vifuatavyo:-

(3) Pale ambapo theluthi mbili ya idadi ya jumla ya Wajumbe haijafikiwa kama inavyotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (2), Mwenyekiti wa Bunge Maalum atabainisha suala au masuala yaliyobishaniwa kwa madhumuni ya kupigiwa kura kwa mara ya pili.

(4) Suala au masuala yaliyobainishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) yatapitishwa na Bunge Maalum kwa kuzingatia kuungwa mkono kwa theluthi mbili ya wajumbe wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya wajumbe wote kutoka Tanzania Zanzibar.

(5) Pale ambapo kuungwa mkono kwa theluthi mbili hakujafikiwa kama inavyotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (4), Bunge Maalum litapiga kura kwa mara ya tatu, na suala au masuala yataamuliwa kwa wingi wa kura za jumla za wajumbe kutoka Tanzania Bara na kwa wingi wa kura za jumla za wajumbe kutoka Tanzania Zanzibar.

(6) Baada ya kupiga kura chini ya kifungu kidogo cha (5), Katiba inayopendekezwa itachukuliwa kuwa imepitishwa na Bunge Maalum na masharti ya Sheria ya Kura ya Maoni yatatumika.

(7) Utaratibu wa kupiga kura chini ya kifungu hiki utakuwa kama utakavyoelezwa katika Kanuni za Bunge Maalum.

Marekebisho ya kifungu cha 27

**9.** Sheria mama inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 27 kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake vifungu vidogo vifuatavyo:-

> "(2) Kutakuwa na uhuru wa maoni katika mijadala ya Bunge Maalum na maoni ya wajumbe hayatahojiwa mahakamani au sehemu yoyote nje ya Bunge Maalum.
>
> (3) Utaratibu wa kuendesha mijadala katika Bunge Maalum utaainishwa katika Kanuni."

Marekebisho ya kifungu cha 28

**10.** Sheria mama inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 28 kwa kuongeza baada ya kifungu kidogo cha (2) kifungu kidogo kifuatacho:

> "(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2), muda ambao Bunge Maalum litajadili Rasimu ya Katiba hautazidi siku sabini kuanzia tarehe ambayo Bunge Maalum lilipoitishwa.
>
> (4) Mwenyekiti wa Bunge Maalum, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, anaweza, kwa ridhaa ya Rais baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar, kuongeza muda uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3) kwa kipindi kitakachofaa kukamilisha shughuli za Bunge Maalum."

**11.** Sheria mama inarekebishwa katika kifungu cha 37 kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kifuatacho:- Marekebisho ya kifungu cha 37

"Kuvunjwa kwa Tume 37.–(1) Baada ya kuwasilishwa kwa Rasimu ya Katiba kwenye Bunge Maalum chini ya kifungu cha 20(3), Rais, kwa amri iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, ataivunja Tume."

Umepitishwa na Bunge tarehe 06 Septemba, 2013.

Dkt. THOMAS D. KASHILILAH,
*Katibu wa Bunge*